# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA ,WAZEE NA WATOTO

**SIMU YA UPEPO: "REGCOM "**
**SIMU NA:- +255783307822**
**Email: sokoinerrh@afya.go.tz**

HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA LINDI
S.L.P. 1011
**LINDI.**

## MKATABA

## WA UJENZI WA JENGO LA WAGONJWA MAHUTUTI

## (ICU)

**MKATABA NA - MOHCDGE/SOKOINERRH/2021/22/6022/W/11**

# FOMU YA MKATABA

Mkataba huu wa ujenzi wa jengo la wagonjwa Mahututi (ICU) Lindi umeiingiwa leo tarehe ..29.... Mwezi ...12.....2021

Kati ya ***LADSLAUS P. SIMAMA WA P.O BOX 118 MASASI*** ambaye katika makubaliano haya atajulikana kama **MWAJIRIWA (FUNDI)** kwa upande mmoja

Na

***MGANGA MFAWIDHI WA HOSPITALI YA MKOA WA LINDI*** ambaye kwa upande mwingine atajulikana kama **MWAJIRI** (Mpokea huduma).

Mwajiri na Mwajiriwa katika mkataba huu wanakubaliana kwa pamoja kuzingatia mambo yafuatayo:

1. Mwajiri anakubali kumwajiri Fundi kufanya kazi zilizoorodheshwa katika kipengele cha pili cha Mkataba huu kwa gharama ya **Tshs 76,800,000.00 (milioni sabini na sita na mia nane elf utu) kwa jengo moja.**

2. Kwamba Mwajiriwa (fundi) atafanya kazi za ufundi zilizoorodheshwa katika nukuu ya bei aliyoomba kama zilivyotajwa katika mkataba huu (kulingana na nukuu ya bei iliyoambatishwa pamoja na muhtasari wa majadiliano):-

3. Vifaa vya ujenzi katika mkataba huu vitanunuliwa na Mwajiri

4. Mwajiriwa/Fundi anakubali kuwa endapo itabainika kuwepo kasoro yeyote ya kiufundi wakati wa ukaguzi au utendaji wa kazi, atalazimika kurekebisha kasoro hizo kwa gharama yake

5. Msimamizi Mkuu na mtaalam wa kazi za mkataba huu atakuwa Mhandisi wa Ujenzi katika Ofisi ya RAS (Meneja wa Mradi)

6. **<u>MUDA WA KAZI</u>:**

   a) Mwajiriwa amekubali kutekeleza mkataba huu kuanzia tarehe ....17.... mwezi....01........ mwaka...2022..., hadi tarehe...30... mwezi ....04.... Mwaka...2022

   b) Mwajiri amekubali kumlipa Mwajiriwa kwa kazi zote atakazofanya sawa sawa na mkataba huu.

## 7. VIAMBATISHO VYA MKATABA

Viambatisho vifuatavyo ndivyo vitakuwa sehemu ya mkataba huu;

a. Fomu ya Mkataba
b. Masharti ya Mkataba
c. Nukuu ya bei ya Mwajiriwa/Fundi
d. Muhtasari wa majadiliano

## MASHARTI YA MKATABA:-

**Kifungu 1: Tafsiri**

Katika Masharti ya Mkataba huu, maneno yafuatayo yatakuwa na maana zilizotolewa kwa maneno hayo kama ilivyo hapa chini:

**Maunzi:** Ni vitu vinavyotumika katika ujenzi (mchanga, mawe, kokoto, saruji, chuma, mbao n.k )

**Mwajiri:** MGANGA MFAWIDHI WA HOSPITALI YA MKOA WA LINDI

**Mhandisi:** Mtu aliyeteuliwa na Mwajiri kuwa meneja wa mradi na kuwa na wajibu wa usimamizi wa kazi na usimamizi wa Mkataba

**Mwakilishi wa Mhandisi:** Watu au mtu aliyeteuliwa/walioteuliwa na Katibu Tawala Mkoa wa Lindi mwenye/wenye wajibu wa kusimamia kazi.

**Fundi :** Taasisi au mshika mkataba ambaye ameingia mkataba na Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Mkoa wa Lindi

**Kazi:** Ni shughuli zinazotakiwa kufanywa na mwajiriwa kulingana na mkataba

**Kifungu 2: Usimamizi wa Kazi:**

Fundi atatekeleza kazi kwa uangalifu na kwa kufuata utendaji unaotakiwa na Mhandisi ili kufikia mahitaji maalumu ya ubora, kiasi na muda uliopangwa. Kama katika wakati wowote ule Mhandisi anaona uzembe, au kubadilika kwa mwelekeo wa utendaji kazi wa fundi, hatua zinazofaa zitachukuliwa ili kurekebisha hali hiyo.

**Kifungu 3: Ukaguzi**

Mhandisi au mwakilishi aliyepewa mamlaka na Mwajiri wana haki ya kukagua kazi, na Fundi atatoa usaidizi kwa shughuli hiyo na kwa wakati atakaohitaji Mhandisi. Iwapo itaonekana kwamba kuna uzembe ulifoanywa na Fundi ambao umesababisha gharama ya mradi kuongezeka, gharama hiyo itakatwa kwenye malipo ya fundi.

**Kifungu 4: Ubora wa Maunzi na Usanifu wa Kazi**

Maunzi yote na usanifu wa kazi vitakuwa na ubora kama ilivyofafanuliwa katika mkataba na pia kulingana na maelekezo ya Mhandisi na vitapimwa kama Mhandisi atakavyoona inafaa. Mwajiri atatoa bure msaada unaohitajika kwa ajili ya kupima ubora wa maunzi na atakuwa na wajibu wa kugharimia upimaji wote utakaohitajika.

**Kifungu 5: Upatikanaji wa Maunzi**

Fundi hatatumia maunzi bila kupata kibali kutoka kwa Mhandisi. Upatikanaji wa maunzi utakuwa ni jukumu la Mwajiri.

**Kifungu 6: Usafishaji wa Eneo la Kazi**

Baada ya kumaliza kazi, Fundi ataondoa kutoka eneo la kazi zana zote, uchafu na mitambo na ataacha eneo la kazi likiwa safi na katika hali itakayokubaliwa na Mhandisi.

**Kifungu 7: Mabadiliko ya Wigo wa kazi**

Kwa idhini ya Mwajiri, Mhandisi anaweza kubadilisha umbo, ubora au kiasi cha kazi na atakuwa na mamlaka ya kumwagiza Fundi ipasavyo. Mabadiliko hayo yatafanywa kwa agizo la Mabadiliko katika Mkataba ambayo yatakuwa yameidhinishwa na Bodi ya Zabuni. Iwapo mabadiliko hayo yataongeza au kupunguza gharama ya mkataba, idhini ya Mwajiri na Bodi ya Zabuni itahitajika.

Kiasi cha fedha kitakachoongezeka kitatokana na kiwango cha kizio au kama hakuna kiwango cha kizio kinachotumika, kiwango cha soko kitatumika kama itakavyoamriwa na Mhandisi na kukubaliwa na wote, Mwajiri na Fundi.

**NA KWAMBA,** Fundi atawajibika kurekebisha kasoro yeyote itakayojitokeza ndani ya kipindi cha miezi sita baada ya kukamilika kwa kazi yake.

### Kifungu 8: Kiasi

Kiasi kilichowekwa kwenye mchanganuo wa Makadirio ya Kazi ni kiasi kilichokadiriwa kwa kazi na kisichukuliwe kuwa ndiyo kiasi sahihi kitakachofanywa na Fundi.
Mhandisi atapima thamani ya kazi halisi iliyofanyika na ataidhinisha gharama halisi ya kazi iliyofanyika kama ilivyofafanuliwa katika Mkataba.

## C: MALIPO

### Kifungu 9: Malipo

a) Gharama ya kazi yote itakuwa kiasi cha shilingi za ki-Tanzania **76,800,000.00 (Milioni sabini na sita mia nane elfu tu)** kwa jengo moja tu.

b) Malipo yatafanyika kwa awamu kulingana na kiwango cha kazi iliyofanyika.

c) Malipo yatafanywa kwa Fundi wakati kazi inaendelea baada ya Mhandisi wa Ujenzi (Project Manager) kukagua, kupima na kuthibitisha viwango/ubora wa kazi iliyofanyika na kutoa hati ya malipo

d) Mwisho wa kazi Mhandisi atatoa cheti kinachoonesha kuwa kazi imekamilika kwa viwango vilivyoainishwa kwenye mkataba.

### Kifungu 10: Kusitisha Mkataba

Mwajiri atakuwa na uwezo wa kusimamisha Mkataba kama upande wa Pili utakuwa umesababisha yafuatayo:-

a) Amekiuka Masharti ya Mkataba
b) Ameshindwa kufika kazini bila taarifa ndani ya siku 7
c) Anapopewa Maelekezo na Mhandisi Mshauri na akakataa kuyatekeleza ndani ya muda aliyopewa
d) Kuwepo Viashiria na vitendo vya ukosefu wa uaminifu kwa upande wa fundi wakati wa utekelezaji wa majukumu yake katika mradi

Mwajiriwa (Fundi) atakuwa na uwezo wa kusimamisha Mkataba kama upande wa Pili utakuwa umesababisha yafuatayo:-

a) Amekiuka Masharti ya Mkataba
b) Endapo Mwajiri atashindwa kumlipa Fundi ndani ya siku 28 baada ya Mwajiri kupitisha madai yake

**Kifungu 11: Usuluhishi wa Matatizo ya Kimkataba**

Iwapo itatokea mgogoro wowote baina ya Mwajiri na Fundi katika utekelezaji wa Mkataba, watakaa kwa pamoja na kusuluhisha mgogoro huo. Iwapo itashindikana katika usuluhishwaji wa mgogoro huo, Mwajiri atachagua mtu wa pili na fundi pia katika kusuluhisha mgogoro huo na endapo itashindikana, Mwajiri na Fundi watakubaliana kuvunja Mkataba.

**Kifungu 12: Majukumu ya Kamati mbalimbali.**

Wajibu mkubwa wa kamati mbalimbali ni kusimamia shughuli zote zinazofanyika katika mradi, kuanzia manunuzi, mapokezi ya vifaa pamoja na usimamizi wa ubora wa kazi. Pia kamati zitakuwa zikitunza taarifa mbalimbali kuanzia za vifaa vyote vilivyopokelewa kwenye eneo la kazi (site) na kuvihakiki na kusajiliwa kwenye rejista iliyo kwenye eneo la mradi. Kufanya vikao shirikishi kujadili maendeleo ya mradi pamoja na changamoto mbalimbali kwenye mradi.

**MKATABA UMESAINIWA NA:**

**Saini** ..................................................... [signature]

**Jina:** DR. MUHSINI K. MOHAMED ..................................................... 29/12/2021

**Cheo: Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Mkoa wa Lindi**

MEDICAL OFFICER INCHARGE
SOKOINE REGIONAL REFERRAL HOSPITAL
P.O.Box 1011
LINDI

**Mbele ya:** 29/12/2021

**Saini:** ............................................. [signature] Shabani

**Jina:** RICHARD A. SHABANI .............................................

**Cheo: Katibu Tawala Msaidizi ~~Miundombinu~~** AFYA

REGIONAL MEDICAL OFFICER
P.O. Box 1011
LINDI

**Cheo: Katibu Tawala Msaidizi Miundombinu**

NA

**Jina:** LADISLAUS .P. SIMAMA

**Cheo: FUNDI**

**Saini:** FUNDI MKUU

LADISLAUS P. SIMAMA
BOX 118.
MASASI

**Saini**.:

**Jina:** RAJABU AHAMADI ISSA

**Cheo: Shahidi wa Fundi**

## SCHEDURE OF LABOURS OF ICU

| Na. | AINA YA KAZI | BEI YA UFUNDI - Shs |
|---|---|---|
| | | |
| A | **Msingi wa Jengo (Sub-structure)** | |
| 1 | Kuseti jengo | 300,000/= |
| 2 | Uchimbaji wa msingi | 500,000/= |
| 3 | Kufukia | 200,000/= |
| | | |
| | **Kufunga mbao** | |
| 4 | Pembezoni mwa jamvi | 200,000/= |
| 5 | Pembezoni mwa nguzo mlalo na wima | 400,000/= |
| 6 | Kuondoa mbao | 200,000/= |
| | | |
| | **Kusuka nondo** | |
| | Kusuka nondo kwenye nguzo mlalo, wima na kitako kwa chini | 700,000/= |
| | | |
| | **Kumwaga zege** | 600,000/= |
| 7 | Chini kwenye msingi wa tofali | 300,000/= |
| 8 | Chini kwenye msingi wa nguzo | 700,000/= |
| 9 | katika nguzo ya awali | 2 |
| 10 | kwenye jamvi | 2,000,000/= |
| 11 | Ujenzi wa tofali (7,134No) | |
| | **Mawe** | |
| 12 | Upangaji wa mawe na utandazaji wa DPM | 1,200,000/= |
| 13 | Umwagiliaji wa maji | 500,000/= |
| | **Jumla ndogo msingi wa jengo** | 9,800,000/= |
| | | |
| B. | **Kunyanyua jengo (Super-structure)** | |
| 1 | Ujenzi wa tofali za kuta na uwekaji DPC (12987No) | 7,500,000/= |
| | **Jumla ndogo kunyanyua jengo** | |
| | | |
| | **Kufunga mbao katika:** | |
| 2 | Nguzo mlalo | 500,000/= |
| 3 | Nguzo wima | 800,000/= |
| | **Kusuka nondo katika:** | |
| 4 | Nguzo mlalo | 400,000/= |
| 5 | Nguzo wima | 600,000/= |
| | **Kumwaga zege katika:** | |
| 6 | Nguzo mlalo | 900,000/= |
| 7 | Nguzo wima | 1,200,000/= |
| 8 | Umwagiliaji wa maji | 300,000/= |
| | **Jumla ndogo kunyanyua jengo** | 12,200,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| | | |
| **C.** | **Kuezeka (Roof structure and covering)** | |
| 1 | Kuezeka na ufungaji wa gata | 6000,000/= |
| | **Jumla ndogo kuezeka jengo** | 6,000,000/= |
| | | |
| **D.** | **Milango na Madirisha** | |
| 1 | Kufitisha fremu za milango | 1,000,000/= |
| 2 | Kufitisha shata za milango pamoja na vitasa | 2,500,000/= |
| 3 | Upakaji wa Varnishi katika milango na fremu | 700,000/= |
| 4 | Ufitishaji wa madirisha ya chuma | 500,000/= |
| | **Jumla ndogo Milango na Madirisha** | 4,700,000/= |
| | | |
| **E.** | **Umaliziaji (Finishing)** | |
| | *Upigaji wa lipu pamoja na kutengeneza koplo:* | |
| 1 | Nje ya jengo | 2,500,000/= |
| 2 | Ndani ya jengo | 3,500,000/= |
| 3 | Ujenzi wa ramp | 1,000,000/= |
| 4 | Ujenzi wa tofali pembezoni mwa msingi kuzunguka jengo | 800,000 |
| 5 | Ujenzi wa meza na kabati | 1,500,000/= |
| | **Sakafu** | |
| 6 | Uwekaji wa sakafu ya kupokea vigae (beds) | 1,500,000/= |
| 7 | Uwekaji wa vigae pamoja na grauti katika sakafu (floor tiles) - pamoja na epoxy | 5,000,000/= |
| | **Jumla ndogo umaliziaji(finishing)** | 16,300,000/= |
| | **Dali:** | |
| 1 | Ufungaji wa mbao za dali (Brandering) | 1,700,000/= |
| 2 | Uwekaji wa dali na mikanda ya gypsum | 2,000,000/= |
| 3 | Uwekaji wa dali ya pvc kuzunguka nyumba kwa nje | 500,000/= |
| 4 | Uwekaji wa vigae katika kuta na upakaji grout | 1,800,000/= |
| | **Jumla ndogo dali** | 6,000,000/= |
| **F.** | **Rangi na Mapambo (Painting & Decoration)** | |
| | **Kupakarangi mikono mitatu pamoja na skimming katika:** | |
| 1 | Kuta za nje | 2,000,000/= |
| 2 | Kuta za ndani | 3,000,000/= |
| 3 | Dali | 1,500,000/= |
| | **Kupaka rangi mikono mitatu katika:** | |
| 4 | Msingi wa nyumba | 500,000/= |
| 5 | Grill za milango na madirisha | 300,000/= |
| | **Jumla ndogo Rangi na mapambo** | 7,300,000/= |
| | | |
| **G.** | **Umeme (Electrical installation)** | |
| 1 | Usukaji wa umeme awamu ya kwanza - Conduit na Box | 1,500,000/= |
| 2 | Usukaji wa umeme awamu ya pili (2nd fix)-fittings | 3,500,000/= |
| | **Jumla ndogo Umeme** | 5,000,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| | | |
| **H.** | **<u>Mifumo ya maji safi na taka (Water Supply and Sewage system)</u>** | |
| 1 | Ufungaji bomba awamu ya kwanza (Kuchimbia bomba) | 1,500,000/= |
| 2 | Ufungaji bomba awamu ya pili (2nd fix) -fittings | 2,500,000/= |
| 3 | Ufungaji wa Mifumo ya maji ya mvua kwenda kwenye tanki | 1,000,000/= |
| | **Jumla ndogo Mifumo ya maji safi na taka** | 5,000,000/= |
| J | **Mfumo wa mtandao(ICT)** | |
| 1 | Ufungaji wa mfumo wa ICT | 4,000,000/= |
| | **Jumla ndogo Mfumo wa ICT** | 4,000,000/= |
| K | **Ufungaji wa mfumo wa Gas** | |
| 1 | Ufungaji wa mfumo wa Gas awamu ya kwanza | 1,500,000/= |
| 2 | Ufungaji wa mfumo wa Gas awamu ya pili | 2,000,000/= |
| | **Jumla ndogo Mfumo wa Gas** | 3,500,000/= |
| L | **Ufungaji wa mfumo wa Ac** | |
| 1 | Ufungaji wa mfumo wa Ac awamu ya kwanza | 500,000/= |
| 2 | Ufungaji wa mfumo wa Ac awamu ya pili | 2,500,000/= |
| | **Jumla ndogo Mfumo wa Ac** | 3,000,000/= |
| | | |
| | **<u>MAJUMUISHO (SUMMARY)</u>** | |
| NA | **MAELEZO** | **Shs** |
| A. | Msingi wa Jengo (Sub-structure) | 9800,000/= |
| | | 12,200,000/= |
| B. | Kunyanyua jengo (Super-structure) | ~~60,00,000/=~~ |
| | | |
| C. | Kuezeka (Roof structure and covering) | 6000,000/= |
| | | |
| D. | Milango na Madirisha | 4,700,000/= |
| | | |
| E. | Umaliziaji (Finishing) | 16,300,000/= |
| | | |
| F. | Rangi na Mapambo (Painting & Decoration) | 7,300,000/= |
| | | |
| G. | Umeme (Electrical installation) | 5000,000/= |
| | | |
| H. | Mifumo ya maji safi na taka (Water Supply and Sewage system) | 5000,000/= |
| I | Mfumo wa mtandao (ICT) | 4,000,000/= |
| J | Mfumo wa mtandao(ICT) | |
| | | |
| K | Ufungaji wa mfumo wa Gas(Medical gas) | 3,500,000/= |
| | | |
| L | Ufungaji wa mfumo wa Ac na ventilation | 3,000,000/= |
| | | |
| | **JUMLA KUU Shs.** | 76,800,000/= |

LADISLAUS P. SIMAMA
BOX 118